# Urasimishaji wa Maneno ya Mkopo kutoka Kiswahili katikaLugha yaKimalila

**Azimio Sote**
Chuo Kikuu Kishiriki cha Katoliki Mbeya
*azimiolaiti@gmail.com*

***Ikisiri***

*Makala haya yamejikita katika kuchambua michakato inayotumika kurasimisha nomino za mkopo katika lugha ya Kimalila [M 24] zinazotoka katika lugha ya Kiswahili kwa kumakinika katika vipengele vya kifonolojia na kimofolojia. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa njia ya hojaji na ushiriki, ambapo jumla ya maneno 312 yalichunguzwa. Makala yameonesha kwamba nomino zote zinazokopwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kimalila ni lazima ziboreshwe walau kwa kuwekewa toni na kiambishi awali tanglizi. Mabadiliko mengine yaliyobainika ni ya udondoshaji na uchopekaji wa sauti pamoja na uambishaji wa maumbo ngeli mawili katika shina moja. Maboresho haya yanafanyika ili yaendane na fonolojia pamoja na mofolojia ya lugha ya Kimalila. Inaonesha kuwa hakuna neno la mkopo kutoka lugha ya Kiswahili linalorasimishwa bila kuboreshwa. Hata hivyo, kuwepo kwa maneno mengi ya Kiswahili katika lugha ya Kimalila kunaweza kuwa na athari katika uhai wa lugha Kimalila. Ipo haja ya tafiti zaidi kufanyika kuhusiana na athari za lugha ya Kiswahili au lugha nyingine katika lugha ya Kimalila.*

**Maneno Muhimu:** Kiswahili, Kimalila, maneno ya mkopo, nomino, michakato ya urasimishaji

## 1.0 Utangulizi

Ni jambo la kawaida lugha kuingiliana na kuathiriana kutokana na wazungumzaji wa lugha kuwa na tabia ya kuchangamana

kwa sababu mbalimbali. Muingiliano huu ni chanzo kimojawapo cha lugha kupitia mabadiliko, yakiwemo ya ukopaji wa maneno, kwa vile suala la mabadiliko katika lugha haliepukiki (Clowley, 1998; Hock na Joseph, 2009; Thomason, 2001). Muingiliano wa lugha unasababisha watu kukopa vipengele mbalimbali vya sarufi kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine kutokana na sababu mbalimbali (Bahumaid, 2015; Campbell, 2004; McMahon, 1994). Kwa mujibu wa Thomason (2001), ukopaji wa maneno katika lugha unahusu nomino zaidi ikilinganishwa na kategoria nyingine za maneno kama vitenzi na vivumishi (Myers-Scotton, 2002; Rendón, 2008; Thomason, 2001).

Maneno yanayokopwa hayakubaliki kwa urahisi kuwa sehemu ya msamiati wa lugha kopaji kutokana na tofauti zinazojitokeza kati ya lugha kopaji na kopwaji (Hock na Joseph, 2009). Kiwango cha kuyakubali maneno ya mkopo kinatofautiana kati ya neno na neno kutokana na sababu mbalimbali (Campbell, 2004; Haspelmath, 2009). Kwa mfano, Haspelmath (keshatajwa) anataja sababu tatu: Mosi, neno lililochukua muda mrefu zaidi litakubalika, ilhali neno lenye muda mfupi litapata upinzani kutoka kwa baadhi ya watumia lugha, hasa wazee, kwa vile litaonekana kuwa ni geni katika maarifa yao.

Pili, kiwango cha muingiliano wa lugha kama ni kikubwa kitasababisha wazungumzaji kuingiza msamiati wa kigeni kwa urahisi zaidi. Hii ina maana kwamba kiwango cha uelewa wa lugha ngeni kinaweza kuamua uwezo wa kupokea msamiati kama ulivyo, au kuufanyia maboresho ili uendane na ruwaza za lugha pokezi. Tatu, mtazamo wa watu kuhusu lugha unaweza kuwafanya waone kuwa lugha moja ni maarufu kuliko lugha

nyingine. Hivyo, wazungumzaji wa lugha isiyo maarufu watashawishika zaidi kukopa maneno kutoka katika lugha wanayoamini kuwa ni maarufu ili waonekane kuwa na wao ni maarufu.Hata hivyo, mabadiliko yanapotokea huwa hayapokelewi kwa mtazamo chanya na watu wote, bali kuna baadhi yao huona kuwa lugha ya mwanzo ni bora kuliko iliyopitia mabadiliko. Vilevile, kuna kundi la watu huamini kuwa kukopa maneno kutoka lugha nyingine ni kero kwao, jambo linalosababisha kugoma kutumia maneno ya mkopo.

## 1.1 Namna ya Kubaini Chimbuko la Neno la Mkopo

Lugha zinaundwa na vipashio mbalimbali, ambavyo wakati mwingine inakuwa vigumu kubaini etimolojia yake kwa vile vinapatikana katika lugha zaidi ya moja. Vipashio hivi vinaweza kuwa vya kifonolojia, kimofolojia, au kisintaksia. Hii imemsukuma Halpemath (2009) kupendekeza njia nne za kubaini uelekeo wa ukopaji wa vipashio katika lugha. Kwanza ni urahisi wa neno kuweza kuchambuliwa kwa urahisi kimofolojia katika lugha. Lugha inayoruhusu kwa urahisi zaidi neno kuchambuliwa kati ya lugha zinazolinganishwa itachukuliwa kuwa ndiyo iliyotoa neno la mkopo. Pili, ikitokea fonolojia inaruhusu mabadiliko kutokea katika lugha A lakini siyo B, basi lugha B itachukuliwa kuwa ndiyo iliyotoa neno au umbo la mkopo. Tatu, ikiwa neno au kipashio kitapatikana katika lugha dada za B lakini haina athari yoyote katika lugha A, basi lugha B itachukuliwa kuwa ni chanzo cha neno la mkopo. Nne, maana inaweza kusaidia kubaini uelekeo wa neno la mkopo pia.

Hata hivyo, Haspelmath (keshatajwa) anatoa angalizo kuwa vigezo hivi wakati mwingine havitoi matokeo sahihi ikiwa

maneno ni ya zamani sana na kuyafanya yaonekane kuwa sehemu ya msamiati asilia wa lugha. Sababu nyingine ni ikiwa maneno yamepitia katika lugha nyingi pamoja na lugha zilizotoa neno la mkopo kuwa nyingi. Licha ya changamoto hizi, bado njia hizi haziwezi kubezwa na kuachwa kuzitumia kutokana na mchango wake.

Maneno yanayokopwa katika lugha hulazimika kuchakatwa ili yaendane na mifumo ya kifonolojia na kimofolojia ya lugha inayokopa. Hata hivyo, lugha zina tabia ya kufanana na hata kutofautiana katika baadhi ya vipengele. Tofauti katika lugha zinaufanya ukopaji kukabiliana na ukinzani katika kukubalika kwa urahisi kutokana na masharti zuizi ya kiisimu yanayoongoza lugha pokezi. Matokeo yake, msamiati unapoingia katika lugha pokezi unalazimika kufuata kanuni na ruwaza za lugha pokezi kupitia urasimishaji kifonolojia na kimofolojia ili yakubalike na watumiaji wa lugha (Lodhi, 2000; Kahigi, 2005; Zivenge, 2009).

## 1.2 Sauti za Lugha ya Kiswahili na Lugha ya Kimalila

Lugha ya Kiswahili ina sauti za konsonanti 27 na irabu tano na viyeyusho viwili (Massamba na wenzake, 2004) na kufanya Kiswahili kuwa na sauti 34. Idadi ya konsonanti imeongezeka kutokana namkuzijumuisha sauti za konsonanti nne zenye mpumuo. Kwa upande mwingine, lugha ya Kimalila [M24], kama ilivyoainishwa na Guthrie (1967-1971), ina sauti za konsonanti 22 ambazo ni: (**p, b, m, β/bh, f, v, t, d, n, s, z, l, sh, ɟ/j, ɲ/ny, tʃ/ch, k, g, ŋ/ng’, x/ kh, ɤ/gh, h**), irabu saba (**i, ɨ, e, a, o, ʉ, u)** na viyeyusho viwili (j/y, w) na kufanya jumla ya sauti kuwa 31 kama zilivyoboreshwa kutoka Kutsch-Lojenga (2007).

Vilevile, Irabu za Kimalila zinaweza kuwa ndefu na kuhesabika kama fonimu pia. Hivyo, lugha ya Kimalila ina jumla ya sauti za irabu 14 (Kutsch-Lojenga, keshatajwa). Sauti /**dh, th, r**/ zinapatikana katika lugha ya Kiswahili, lakini hazipatikani katika Kimalila kama ilivyo kwa sauti /**bh, kh**/ zinazopatikana katika Kimalila ingawa hazipatikani katika Kiswahili.

## 1.3 Nadharia

Nadharia mbili zimetumika katika makala hii: nadharia masharti zuizi na mikakati boreshi pamoja na nadharia ya usilimisho. Nadharia masharti zuizi na mikakati boreshi iliyoasisiwa na Paradis na Lacharite (1997) inaeleza kwamba maneno yanayokopwa hayapokelewi kwa urahisi na lugha inayokopa kutokana na baadhi ya tofauti za kifonolojia zinazojitokeza kati ya lugha kopaji na inayokopwa. Hivyo, neno la mkopo linalazimika kuboreshwa ili liweze kuendana na fonolojia ya lugha inayokopa (Haspelmath, 2009; Hock & Joseph 2009; McMahon, 1994). Nadharia hii inaongozwa na kanuni nne.

Mosi, sauti katika neno linalokopwa zinapaswa kubaki zilivyo badala ya kuzidondosha. Pili, sauti katika neno zifanyiwe maboresho kwa kuzingatia hatua chache zaidi. Hivyo, ikiwa hatua zitazidi mbili, udondoshaji ufanyike. Tatu, wakati wa udondoshaji au uchopekaji, kipaumbele kiwe kwenye uwekevu katika athari. Hii ina maana kwamba mchakato wenye athari chache zaidi ndiyo utakaoruhusiwa kufanyika. Nne, ikiwa kuna ukiukaji wa masharti zuizi mawili au zaidi, kipaumbele kiwe kwenye kiwango cha juu cha kifonolojia. Hivyo, utatuzi wa tatizo kubwa zaidi uzingatiwe kwanza. Nadharia hii ni ya muhimu kwa kuwa inafafanua sababu za mabadiliko ya

kifonolojia kutokea katika maneno ya mkopo. Vilevile, nadharia hii inaonesha sababu ya baadhi ya maneno kutobadilika. Hata hivyo, mbinu hii haiwezi kutumika kuelezea mabadiliko ya kimofolojia.

Kwa upande mwingine, nadharia ya usimilisho imetumika. Nadharia hii inajengeka katika msingi kwamba lugha zinapoingiliana kwa muda mrefu ni kawaida kuathiriana (Campbell, 2004; Lusekelo, 2019). Hivyo, kunakuwa na uwezekano wa msamiati kutoka lugha moja kuingia katika lugha nyingine. Msamiati unaoingizwa katika lugha nyingine unafanywa kuwa sehemu ya msamiati wa lugha pokezi. Tabia hii ndiyo inayoitwa usimilisho. Nadharia hii ya usilimisho imetumika katika uchambuzi wa data za kimofolojia kwa vile nadharia ya masharti zuizi na mikakati boreshi imemakinikia fonolojia zaidi.

## 2.0 Methodolojia

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa njia za hojaji na ushiriki. Katika mbinu ya hojaji kulikuwa na hojaji mbili. Hojaji ya kwanza ilikuwa na maswali funge yaliyomtaka mtoataarifa kutaja maneno yanayohusu vitu, vyeo, watu, mavazi tabia na mahusiano kwenye mikitadha ya siasa, shuleni au vyuoni, hospitalini, katika dini, mawasiliano ya simu, biashara, kilimo, na usafirishaji. Maeneo haya yalichukuliwa kuwa yana matumizi mengi ya maneno ya kigeni kwa vile, mara nyingi, yanashughulika na mambo ambayo siyo ya asili katika lugha ya Kimalila. Hojaji ya pili ilikuwa na sentensi fupi 30 ambapo kulikuwa na nomino za umoja na uwingi kwa lengo la kubaini muundo wa nomino na ngeli za majina.

Mbinu nyingine iliyotumika ilikuwa ya ushiriki ambapo mtafiti alishiriki katika mazungumzo na wazawa wa lugha ya Kimalila katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo kwa njia ya simu. Hii iliwezekana kwa kuwa mtafiti ni mzawa wa lugha ya Kimalila. Hivyo, mtafiti aliweza kukusanya nomino mbalimbali, alizodhani kuwa, ni za kigeni. Mbinu hizi (za hojaji na ushiriki) zilikuwa zinategemeana kwa kuwa kila moja ilikuwa na ubora wake pamoja na upungufu uliohitaji kufidiwa na mbinu nyingine. Kwa mfano, mbinu ya ushiriki ilimwezesha mtafiti kupata maneno pamoja na matamshi yake ambayo isingekuwa rahisi kuyapata katika hojaji pekee. Mbinu hizi zilimuwezesha mtafiti kukusanya nomino 543 kutoka katika makundi mbalimbali ya matumizi. Nomino zilizokusanywa zilipitiwa na wazawa wanne wa lugha ya Kimalila wenye umri kati ya miaka 45 na 55 ili kubaini kama ni za asili katika lugha ya Kimalila. Vilevile, mtafiti alilazimika kuyapitia maneno yaliyokusanywa kwa lengo la kubaini kama yapo yenye asili ya Kibantu. Hivyo, maneno yenye asili ya Kibantu yaliondolewa na kubaki nomino 312. Uchakataji wa data ulifanyika kwa kulinganisha neno la asili katika Kiswahili na neno la mkopo katika Kimalila kwa lengo la kubainisha kufanana pamoja na tofauti za kifonolojia na kimofolojia.

## 3.0 Matokeo ya Utafiti

### 3.1 Urasimishaji Kifonolojia wa Maneno ya Mkopo katika Lugha ya Kimalila

Lugha ya Kimalila, kama zilivyo lugha mbalimbali (McMahon, 1994; Ngunga, 2002; Bahumaid, 2015; Msuya na Mreta, 2018; Lusekelo, 2018), ina tabia ya kukopa maneno kutoka katika lugha nyingine. Kwa mujibu wa Hock na Joseph (2009),

urasimishaji wa maneno ya mkopo, kwa kiwango kikubwa, unahusisha michakato ya kifonolojia ili kuyafanya maneno yatamkike kwa urahisi katika lugha inayokopa. Inaonesha kwamba maneno yanayokopwa kutoka lugha ya Kiswahili sharti yapitie mabadiliko kwa viwango tofauti ili yaendane na kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha ya Kimalila. Sehemu ifuatayo inachambua michakato ya kifonolojia inayohusika katika kurasimisha maneno ya mkopo kutoka katika lugha ya Kiswahili yanayoingizwa kwenye lugha ya Kimalila.

### 3.1.1 Mabadiliko ya sauti

Lusekelo (2018) anadokeza kuwa lugha ya Kiswahili imekopa baadhi ya maneno na sauti zake kutoka katika lugha za kigeni kama Kiingereza na Kiarabu ambazo ni ngeni katika lugha za Kibantu. Sauti hizi ni moja ya vyanzo vya tofauti zinazotokea kati ya lugha ya Kiswahili na baadhi ya lugha za Kibantu. Ni kwa msingi huo, lugha Kiswahili ina baadhi ya sauti ambazo hazipatikani katika lugha ya Kimalila kama vile: */dh/*, */th/* na */r/*, kama ilivyo kwa lugha ya Kimalila ambayo ina baadhi ya sauti ambazo hazipatikani katika lugha ya Kiswahili. Maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kiswahili yanayoingizwa katika lugha ya Kimalila yanayokosa sauti mwenza katika lugha ya Kimalila hulazimika kubadilishana nafasi na sauti ambazo zinakaribiana sifa za kimatamshi katika lugha ya Kimalila. Hii ni kutokana na wazungumzaji wa lugha ya Kimalila kushindwa kutamka sauti ambazo hazipo katika kundi la sauti za Kimalila.

**Jedwali la 3.1: Mabadiliko ya Konsonanti kutoka Lugha ya Kiswahili kwenda Lugha ya Kimalila**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa mabadiliko ya sauti (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Barabara | r > l | *ɨ̂mba**l**aba**l**a* |
| **2.** | Ramani | *r* > l | ***ɨ̂l**amani* |
| **3.** | Thumuni | *th*> s | *ɨ̂**s**umuni* |
| **4.** | Thamani | *th*> s | *ɨ**s**aámani* |
| **5.** | Dhamana | *dh > z* | *ɨ**z**ama̋na* |
| **6.** | Kisu | *k>sh* | *ɨ**sh**ɨ̂su* |
| **7.** | Chombo | *ch>sh* | *ɨ**sh**ómbo* |
| **8.** | Kabeji | *b > bh* | *ɨkáabhɨki* |

Mifano kutoka Jedwali la 3.1 inaonesha kuwa sauti *k/ch* zinabadilika kuwa */sh/*, *dh* inakuwa /z/, /*th*/ inakuwa /s/ na sauti /r/ inakuwa /l/. Mabadiliko ya sauti /*dh*, *th* na *r*/ ni thabiti na ni tabirifu kwa kuwa sauti hizi hazipo katika Kimalila. Sauti /*k*/ na /*ch*/ ni fonimu katika lugha ya Kimalila na zinatumika pia. Kwa mfano, neno *kata* (eneo la utawala) linatamkwa *ɨkáata* ambapo */k/*; katika neno *ɨchókho* "choo" sauti /ch/ imetumika pia. Hii ina maana kwamba utokeaji wa sauti */sh/* badala ya */k /* na */ch/* hautabiriki.

Mabadiliko mengine yanahusisha sauti za irabu. Mabadiliko ya kwanza ni ya irabu za juu mbele /i/ kubadilika kuwa irabu ya kati mbele /e/. Vilevile kinyume chake ni mabadiliko ya irabu /e/ kuwa /i/. Mabadiliko haya yanatokana na mvutano wa irabu unaochochewa na sauti inayosababisha mabadiliko kutokea kabla au baada ya sauti inayobadilika. Kwa mfano, irabu /i/ > e katika neno (1) kutokana na irabu /o/ katika neno *polisi* kuwa

ya kati. Hivyo, mvutano huu unasababisha irabu ya juu mbele /i/ iwe ya kati pia.

**Jedwali la 3.2: Mabadiliko ya Irabu kutoka Lugha ya Kiswahili kwenda Lugha ya Kimalila**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa mabadiliko ya sauti (>) | Neno la mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Pol**i**si | i >e | *ʉpóol**e**si* |
| **2.** | Ml**i**ngoti | i>o | *ɨl**óo**ngoti* |
| **3.** | Mkat**e** | e>i | *ɨkáat**i*** |
| **4.** | Kab**e**ji | e >i | *ɨ̂kaabh**ɨ**kɨ* |
| **5.** | Of**i**si | i >e | *ɨnhóf**e**si* |
| **6.** | B**u**stani | u > o | *ɨ̂b**o**sitani* |
| **7.** | Mjer**u**mani | u > e | *ʉmʉjél**e**mani* |

Irabu /u/ inabadilika kuwa /o/ au /e/ kutegemeana na mazingira ya irabu iliyosababisha usilimisho kutokea. Neno *bustani* linakuwa *ɨ̂bositani* /u>o/. Irabu /u/ ni ya juu nyuma, inawezekana inasababisha ugumu katika utamkaji. Kwa mfano, katika neno *ɨ̂b**o**sitani* kuna irabu za juu, kati, juu, chini na juu tofauti na kama ingekuwa *ɨ̂bʉsitani* na kama ingekuwa juu, juu, juu, chini na juu chenye ugumu wa kutamka. Hivyo, irabu /u/ inalazimika kubadilika kuwa ya mbele kati /e/ ili kurahisisha utamkaji. Urahisi huu unatokea pia katika neno *Mjerumani* linalokuwa *ʉmʉjélemani* ambapo irabu /u/ imebadilika kuwa /e/. Hii inatokana na athari za irabu ya kati mbele /e/ inayotangulia kutokea kabla ya /u/ katika shina (-jerumani).

### 3.1.2 Urefushaji irabu

Lugha ya Kimalila ni miongoni mwa lugha zenye irabu ndefu na fupi, ilhali Kiswahili kina irabu fupi tu. Kuna baadhi ya sauti za irabu kwenye nomino za Kiswahili zinazoingizwa kwenye lugha ya Kimalila zinalazimika kurefushwa ili kuendana na kanuni za kifonolojia za lugha ya Kimalila inayoruhusu irabu ndefu.

**Jedwali la 3.3: Urefushaji Irabu**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa urefushaji irabu (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | V**o**da | > | *ɨv**oó**da* |
| **2.** | G**a**ri | > | *ɨg**áa**li* |
| **3.** | P**i**pa | > | *ip**íi**pa* |
| **4.** | N**a**ne | > | *ʉn**áa**ne* |
| **5.** | S**i**mu | > | *is**íi**mu* |

Mifano kutoka katika Jedwali la 3.3 inaonesha kwamba urefushaji wa irabu unafanyika katika irabu ya pili kutoka mwishoni katika maneno ya lugha ya Kimalila, maneno ya Kiswahili yanapokuwa na silabi mbili. Hata hivyo, katika baadhi ya mazingira urefushaji wa irabu haufanyiki, badala yake toni panda huwekwa katika irabu iliyo katika silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno. Hii hufanyika kwa sharti kwamba urefushaji irabu ufanyike katika kiambishi awali tangulizi.

**Jedwali la 3.4: Urefushaji Irabu**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa urefushaji irabu (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Saba | > | *ʉʉsába* |
| **2.** | Debe | > | *ɨɨdébe* |
| **3.** | Mji | > | *uumúji* |
| **4.** | Hela | > | *ɨɨhéla* |

Aidha, urefushaji irabu katika Jedwali la 3.4 hauwezi kufanyika kama katika Jedwali la 3.3 wala mchakato wa urefushaji irabu katika Jedwali la 3.3 hauwezi kutokea kama katika Jedwali la 3.4. Kwa mfano, neno *pipa* katika Jedwali la 3.3(3) haliwezi kuwa **iipî́pa* wala neno *debe* Jedwali la 3.4(2) haliwezi kuwa **ɨ̂́deebe*. Inawezekana kuwa lengo la urefushaji ni kudhibiti kiwango cha chini cha mora 4 katika neno. Hizi ni baadhi ya tofauti zinazopatikana ndani ya lugha ya Kimalila zinazoamua ukubalifu wa neno la kigeni kuingia katika msamiati wake. Tofauti hizi zinashadidia hoja ya Hyman (2003) kuwa kuna baadhi ya tofauti za kimofolojia zinatokea ndani ya lugha za Kibantu.

### 3.1.3 Uchopekaji wa sauti

Lugha ya Kimalila, kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu, hairuhusu mfuatano wa konsonanti au irabu kutokea katika neno. Hivyo, uchopekaji wa sauti hutumika kama njia mojawapo ya kuikabili miundo migeni inayopatikana katika maneno yanayokopwa kutoka katika lugha ya Kiswahili.

#### 3.1.3.1 Uchopekaji wa sauti mwanzoni mwa neno

Kuna baadhi ya nomino za Kiswahili zinazoanza na irabu, ilhali lugha ya nomino za lugha ya Kimalila huanza na konsonanti tu. Nomino za Kiswahili zinazoanza na irabu zinapoingizwa katika lugha ya Kimalila zinalazimika kufanyiwa maboresho kwa kuchopeka konsonanti mwanzoni mwa neno. Uchopekaji huu unafanyika kwa namna mbili. Mosi, ni kwa kuchopeka sauti ya kiyeyusho mwanzoni mwa nomino za Kiswahili zinazoanza na irabu. Pili, ni kwa kuchopeka konsonanti ng'ong'o mwanzoni mwa nomino iliyokopwa katika lugha ya Kiswahili. Maneno yanayoanza na irabu /u/ yanachopekwa sauti /ghw/ (katika Jedwali la 3.5, namba moja na mbili), ambapo kuna konsonanti kwamizi /gh/ inayofuatwa na kiyeyusho /w/. Inawezekana, kuna matukio mawili yametokea. Kwanza ni kuchopeka kiyeyusho /w/, ambacho Rugemalira (2005) amekiita sauti ya miujiza. Pili, kuna kuchopeka kikwamizi cha king'ong'o /gh/ kwa lengo lakurahisisha utamkaji wa kiyeyusho /w/.

**Jedwali la 3.5: Uchopekaji wa Sauti Mwanzoni mwa Maneno ya Mkopo**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa uchopekaji wa sauti (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Uzi | > | *ʉ́**-ghw**ʉzi* |
| **2.** | Upendo | > | *ʉ́**-ghw-**upendo* |
| **3.** | Askofu | > | *U-**ghw-**asikofu* |
| **4.** | Amani | > | ***ɨ̂-y-**amani* |

Katika mazingira mengine king'ong'o /n/ kinachopekwa mwanzoni mwa maneno ya mkopo kutegemeana na sifa za sauti ya konsonanti inayotokea mwanzoni mwa nomino ya mkopo.

**Jedwali la 3.6: Uchopekaji wa Sauti Mwanzoni mwa Maneno ya Mkopo**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa uchopekaji wa sauti (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Funguo | > | ***ɨ-n****fúnkulo* |
| **2.** | Komeo | > | *[ɨ-****ŋn****kómeyo]* |
| **3.** | Sahani | > | ***ɨ̂-n****sanhani* |
| **4.** | Pilipili | > | ***ɨ̂-m****pilipili* |
| **5.** | Blauzi | > | ***ɨ̂-m****bulaghwuzi* |

Mifano hiyo inaonesha kwamba king'ong'o */n/* kinachopekwa mwanzoni mwa sauti */f/, /s/* na kipasuo cha kaakaa laini */k/*. Sauti ya king'ong'o /m/ huchopekwa mwanzoni mwa mashina ya nomino yanayoanza na sauti za midomo */b/*au*/p/* kama katika Jedwali la 3.6(4-5). Hii ina maana kwamba sauti /n/ inaathiriwa na sauti zisizo za midomo.Aidha, uchopekaji mwingine unahusu silabi katika neno la mkopo.

**Jedwali la 3.7: Uchopekaji wa Sauti Mwanzoni mwa Maneno ya Mkopo**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa uchopekaji wa sauti (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Embe | > | ***ɨ̂-ly****-embe* |
| **2.** | Pini | > | ***ɨ̂-nya****-pini* |

Katika Jedwali la 3.7, neno la kwanza, silabi $li$ imechopekwa katika muundo wa ndani. Mageuzi ya uyeyushaji yamesababisha irabu /i/, iliyo katika silabi $li$, kubadilika kuwa kiyeyushi /y/ na kufanya silabi $li$ kuwa $ly$. Halikadhalika, neno la pili katika Jedwali la 3.7linapokea uchopekaji wa silabi $nya$. Uchopekaji huu unazidi kuipa nguvu hoja kuwa silabi mbili katika lugha ya Kimalila hazivumiliki, hivyo, inabidi ziongezwe kwa kuchopeka ilabu au silabi nyingine ili ziwe nne katika neno.

### 3.1.3.2 Uchopekaji katikati ya neno

Lugha ya Kiswahili ina tabia ya kuruhusu sauti za irabu au konsonanti kufuatana katika nomino kama ilivyo kwa baadhi ya lugha za Kibantu. Hata hivyo, lugha ya Kimalila hairuhusu mfuatano huu kutokea. Hivyo, ikiwa sauti za konsonanti zitafuatana, sauti ya irabu italazimika kuchopekwa katikati, ilhali irabu zinapofuatana konsonanti au kiyeyusho kitachopekwa ili kuondoa mfuatano huu usiokubalika.

**Jedwali la 3.8: Uchopekaji wa Sauti-irabu katikati ya Neno**

| **Na.** | **Kiswahili** | **>** | **Neno la Mkopo** |
|---|---|---|---|
| **1.** | Plastiki | > | *__ɨ̂__-p__u__las__i__ki* |
| **2.** | Hospitali | > | *__ɨ̂__-s__ɨ__pitali* |
| **3.** | Askofu | > | *ʉ́-ghwas__i__kofu* |
| **4.** | Biblia | . | *__ɨ̂__-bib__i__li__y__a* |

Mifano hapo juu inaonesha kwamba sauti za konsonanti zimefuatana katika lugha ya Kiswahili, lakini mfuatano huu umetanzuliwa kwa kuchopeka sauti za irabu katikati ya konsonanti kwenye lugha ya Kimalila. Kwa mfano, neno la

kwanza katika Jedwali la 3.8, mifuatano ya konsonanti ya /*pl/*na*/st/* imetanzuliwa kwa kuchopeka irabu */u/* na /i/ mtawalia.Aidha, mfuatano wa irabu unatatuliwa kwa kuchopeka sauti ya konsonanti au kiyeyusho.

**Jedwali la 3.9: Uchopekaji wa Sauti-konsonanti katikati ya Neno**

| Na. | Kiswahili | > | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Taa | > | *ɨ-táa**l**a* |
| **2.** | Sikukuu | > | *ɨ̂-shiku**lu**ku**l**u* |
| **3.** | Pazia | > | *ɨ̂-pazi**y**a* |
| **4.** | Ndoana | > | *ɨ̂-ndo**ghw**ani* |
| **5.** | Suruali | > | *ɨ̂-nsulu**bh**ale* |

Mifano hiyo inaonesha kwamba mfuatano wa irabu */aa/* katika neno la kwanza umetatuliwa kwa kuchopeka konsonanti */l/*, ilhali mfuatano wa irabu */oa/* umeboreshwa kwa kuchopeka kiyeyusho */ghw/*. Hata hivyo, katika neno la mkopo*ɨ-taa**l**a* kutoka kwenye neno la Kiswahili*"taa",* urefushaji wa irabu umefanyika kwa kuwa kuna mora mbili kama ilivyojadiliwa katika Jedwali la 3.9(1). Hivyo, mora mbili zinaonekana kuwa ni tofauti na irabu ya mwisho /taa.a/ jambo linaloruhusu uchopekaji wa konsonanti /l/ kufanyika.

Kwa upande mwingine, kuna baadhi ya nomino za mkopo zinaonesha kuwepo kwa mifuatano ya sauti, ambayo ikichunguzwa kwa kulinganisha na maneno asilia katika lugha ya Kiswahili, inaonesha kwamba kuna mabadiliko mengi yametokea, ikiwemo uchopekaji sauti. Hata hivyo, sauti iliyochopekwa au zilizochopekwa haziwi wazi kwa kuwa

nomino iliyopo inakuwa katika muundo wa nje jambo linaloashiria kuwa uchopekaji sauti umefanyika katika muundo wa ndani.

**Jedwali la 3.10: Uchopekaji wa Sauti katikati ya Nomino**

| Na | Kiswahili | Muundo wa ndani | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Kofia | *[ɨnkof-**ue**-l-a]* | *ɨ̂nkofwela* |
| **2.** | Blanketi | *[ɨmb-**ue**-lengeti]* | *ɨmb**we**lengeti* |
| **3.** | Mlango | *ʉmʉl-**i**-ango]* | *ʉmʉlyango* |

Michakato zaidi ya mmoja imetokea katika (10), ambapo uchopekaji wa sauti katikati ya nomino umetokea. Baadhi ya mabadiliko yanahusisha hatua nyingi kama katika neno *ɨ̂nkofwela* "kofia.":

i. Chopeka king'ong'o /n/ mwanzoni mwa neno la mkopo kofia kupata *[ɨ̂-**n**kofia]*
ii. Badilisha irabuya juu mbele /i/ kuwa ya juu nyuma /u/ kupata neno *[ɨ̂-nkof-**u**-a]*
iii. Chopeka sauti ya kati mbele /e/ baada ya irabu /u/ kupata neno *[ɨ̂-nkof-**ue**-a]*.
iv. Chopeka konsonanti /l/ kati ya /ue/ na /a/kupata neno [*[ɨ̂nkof-ue-**l**-a]*.
v. Yeyusha mfuatano wa sauti /ue/ kupata neno*[ɨ-nkof-**we**-l-a]*.

Mabadiliko matano yametokea katika Jedwali la 3.10(1) bila udondoshaji kutokea. Hata hivyo, hatua hizi tano zinakinzana na dai kuwa mabadiliko yakizidi mawili wakati wa kurasimisha neno la mkopo yatakuwa mengi zaidi, hivyo udondoshaji

utalazimika kutokea (Paradis na Lacharite, 1997). Huu ni upekee katika lugha ya Kimalila.

### 3.1.4 Udondoshaji wa sauti

Udondoshaji katika neno unaweza kutokea mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno. Udondoshaji ni njia mojawapo inayotumika kuikabili miundo ya nomino za Kiswahili inayokuwa na irabu mwanzoni ili ikubalike katika Kimalila.

**3.11: Udondoshaji wa Sauti**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa sauti inayodondoshwa (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | **U**tingo | > | *ʉ-tı́ingo* |
| **2.** | **A**ndazi | > | *ɨ́-ndaanzi* |
| **3.** | **I**shirini | > | *ú-shiliini* |
| **4.** | **U**jamaa | > | *ʉ-ghwʉjáma* |

Udondoshaji umefanyika katika Jedwali la 3.11(1-3), tofauti na ilivyo katika Kiswahili ambapo nomino zinaanza na irabu. Inawezekana udondoshaji unatokea kwa lengo la kuepuka mgongano wa kiambishi awali tangulizi ambacho, katika muktadha huu, ni lazima kitokee. Kwa mfano, neno **ʉ́ʉtingo* katika Jedwali la 3.11(1) halikubaliki kutokana na kutotamkika kirahisi na halizingatii uwekevu kama ilivyo kwa neno *ʉtı́ingo.* Kwa upande mwingine, urefushaji wa irabu katika shina la nomino umefanyika ili kufidia nafasi iliyoachwa wazi na irabu iliyodondoshwa. Hii ni tofauti na 3.11(4), ambapo matukio mawili tofauti yamefanyika bila kuruhusu urefushaji wa irabu. Mosi, ni udondoshaji wa irabu */a/*mwishoni mwa neno na pili ni

uchopekaji wa sauti */ghw/* ili kuzuia irabu ya mwanzo kudondoshwa kama ilivyofanyika katika Jedwali la 3.11(1-3) unaoweza kufanya mora kubaki tatu (*ghwʉ-jama*), ambazo hazivumiliki.

Udondoshaji kati ni aina nyingine ya udondoshaji inayotumika kurasimisha nomino za Kiswahili katika Kimalila. Kwa mfano, kuna neno la Kiswahili: Baiskeli>*ɨbáa-sikeli.* Katika neno hilo la Kiswahili, irabu /i/ imedondoshwa na kusababisha nomino *ɨbáasikeli* kupatikana. Katika neno la mkopo *ɨbáasikeli* limelazimika kuwa na irabu ndefu kwa lengo la kufidia irabu iliyodondoshwa katika neno *baiskeli.* Katika muktadha huu, udondoshaji irabu /i/ badala ya kuchopeka konsonanti au kiyeyusho kama ilivyojadiliwa hapo mwanzo, huenda udondoshaji na urefushaji vimekubalika kwa kuwa neno lina silabi nyingi (tano) katika muundo wa ndani.

Aidha, kuna baadhi ya nomino za Kiswahili zinazoishia na irabu ya chini */a/* mbili, ambazo katika lugha ya Kimalila, inaelekea kuwa zinachukuliwa kuwa ni irabu mbili tofauti badala ya irabu ndefu kama ilivyoripotiwa katika Jedwali la 3.11. Mfuatano wa irabu hizi haukubaliki katika Kimalila, jambo linalosababisha urasimishaji wa nomino kwa njia ya udondoshaji wa irabu ya mwisho kutokea.

**Jedwali la 3.12: Udondoshaji wa Irabu ya Mwisho**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa udondoshaji wa irabu ya mwisho> | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Motoka**a** | > | *ɨ̂mootoka* |
| **2.** | Gita**a** | > | *igɨ̂id*a |
| **3.** | Ujama**a** | > | *ʉ́ghwujama* |
| **4.** | Karatasi | > | *ɨ̂kalata* |

Katika mifano ya hapo juu, udondoshaji wa irabu /a/ umefanyika; urefushaji wa irabu umefanyika pia ili kuziba pengo lililoachwa wazi baada ya udondoshaji kutokea. Kwa upande mwingine, katika Jedwali la 3.12(4), udondoshaji wa silabi *$si$* umefanyika pia ambapo neno *karatasi* limekuwa *ɨ̂kalata*. Hii inaweza kusababishwa na nadharia mbili: kwanza, sauti [s] ni dhaifu hivyo kuruhusu silabi \$si\$ kudondoshwa kwa urahisi. Pili, udondoshaji umekubalika kwa vile neno lina mora nne zinazokubalika. Hivyo, udondoshaji wa silabi \$si\$ unakubalika. Hata hivyo, tofauti na data katika Jedwali la 3.12 (1-3), kuna ughairi kwa baadhi yamaneno, ambayo yamekopwa bila kufanyiwa maboresho yoyote ya udondoshaji wala uchopekaji, tazama Jedwali la 3.13.

**Jedwali la 3.13: Udondoshaji wa Irabu**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa udondoshaji wa irabu (>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Baa | > | *ɨ̂-baa* |
| **2.** | Mkaa | > | *ʉ́-mʉkaa* |

Inawezekana kuwa maneno tajwa katika data ya Jedwali la 3.13 hayajaathirika kwa kuwa bado yanatumiwa na watu wenye athari kubwa ya lugha ya Kiswahili. Hii inatokana na ukweli

kuwa *baa* hazijaenea katika maeneo mengi ya watumia lugha ya Kimalila. Vilevile, neno *ámalasha*, *ambalo* ni la asili katika Kimalila linatumika pia badala ya neno *mkaa*. Hivyo, maneno *ɨ́baa*na*ʉ́mukaa* yanatumiwa na wazungumzaji, ambao ni rahisi kulipokea neno lilivyo bila ya kuliboresha.

### 3.1.5 Uyeyushaji

Uyeyushaji unatumika pia katika lugha ya Kimalila kuchakata maneno ya mkopo ili yaendane na mfumo wa silabi za lugha hii. Imebainika kuwa unafanyika katika muundo wa ndani kunapotokea uchopekaji wa irabu unaosababisha irabu kuandamiana. Hivyo, mfuatano huu wa irabu unatanzuliwa kwa njia ya uyeyushaji. Turejelee mfano uliotolewa katika Jedwali la 3.10(3) tunapotazama neno: Mlango (Kiswahili), ambalo muundo wake wa ndani ni *[úmul-**i**-ango] na* Kimalila ni *Umulyango.*

Katika neno *mlango* inaonesha kwamba kuna uchopekaji wa irabu ya juu mbele /i/ katika muundo wa ndani. Hii ina maana kwamba wazungumzaji wa lugha ya Kimalila wanalipokea neno hili kuwa lina muundo wa *mliango* katika Kimalila tofauti na lilivyo katika lugha ya Kiswahili. Zaidi pia, inaonesha kuwa lugha ya Kimalila ina tabia ya kuchopeka irabu mbili tofauti pia katika muundo wa ndanizinazosababisha uyeyushaji kufanyika. Kwa mfano, neno blanketi linakuwa *[imb**ue**lengeti]* linalozaa neno *imb**w**elengeti*.

### 3.1.6 Toni

Lugha ya Kimalila ni lugha ya toni (Kutsch-Lojenga, 2007) kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu kama vile Kinyamwezi (Maganga na Schadeberg, 1992), Kinyambo (Rugemalira, 2005) na Kibena (Morrison, 2011) zilizo na toni. Hii ni tofauti na lugha ya Kiswahili, ambayo ina tabia ya kutumia mkazo katika silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno (Kihore na wenzake, 2001). Kwa mantiki hii, nomino zinazorasimishwa katika lugha ya Kimalila zinalazimika kufuata fonolojia ya Kimalila kwa kuziwekea toni kutegemeana na muundo wa neno kwa lengo la kurahisisha utamkaji wake. Kwa mfano, neno: Tisa (Kiswahili) linakuwa *ʉʉtísa* (Kimalila).

Mfano uliotolewa unaonesha kwamba neno *ʉʉtísa* limefanyiwa maboresho kwa kuwekewa toni. Suala la toni limetokea katika mifano mbalimbali katika makala haya, ambapo toni zimewekwa katika maneno ya mkopo katika Kimalila.

### 3.1.7 Mabadiliko ya kimofolojia

Lugha za Kibantu zina tabia ya kufanana na kutofautiana kimofolojia. Kuna tofauti zinazotokea kati ya lugha na lugha na nyingine ndani ya lugha moja (Hyman, 2003). Lugha za Kiswahili na Kimalila haziwezi kuepuka tofauti hizi. Hivyo basi, mabadiliko katika nomino zinazokopwa kutoka lugha ya Kiswahili na kuingia katika lugha ya Kimalila hayaepukiki. Sehemu zifuatazo zinamakinika katika kuchambua mabadiliko ya kimofolojia yanayotokea wakati wa urasimishaji maneno ya mkopo katika Kimalila:

### 3.1.7.1Mabadiliko ya muundo wa nomino

Lugha ya Kimalila ina muundo wa nomino wa *kiambishi awali tangulizi* + *umbo ngeli* + *shina* au *kiambishi awali tangulizi* + *shina* (Kutsch-Lojenga, 2007) kama ilivyo kwa baadhi ya lugha za Kibantu. Hii ni tofauti na lugha ya Kiswahili yenye muundo wa *ngeli* + *shina* au *shina pekee*. Hivyo, nomino zinazokopwa kutoka katika lughaya Kiswahili zinalazimika kuambishwa kiambishi awali tangulizi ili ziendane na muundo wa nomino za Kimalila.

**Jedwali la 3.14: Mabadiliko ya Muundo wa Nomino**

| Na. | Kiswahili | Mwelekeo wa muundo wa nomino(>) | Neno la Mkopo |
|---|---|---|---|
| **1.** | Katibu | > | *ʉ́-katibu* |
| **2.** | Kikombe | > | *ɨ̂-shɨkombe* |
| **3.** | Madiwani | > | *á-bhadighwani* |
| **4.** | Jembe | > | *ɨ-jéembe* |

Mifano hiyo inaonesha kwamba lugha ya Kimalila haikopi neno na muundo wake, bali hukopa neno na kulifanyia maboresho ili liendane na mofolojia yake. Hii imebainika pia kwa nomino zenye umbo ngeli kapa katika Jedwali la 3.14(4), ambayo imelazimika kukopwa kama zilivyo, lakini kwa kuweka kiambishi awali tangulizi bila umbo ngeli. Hii ina maana kwamba shina peke yake au shina na umbo ngeli hukopwa kisha kiambishi awali tangulizi huambishwa. Vilevile, inaonesha kuwa uambishaji wa kiambishi awali tangulizi ni suala lisiloepukika katika urasimishaji wa nomino za mkopo katika Kimalila.

### 3.1.7.2Mpishano wa ngeli za majina

Ngeli za majina katika lugha za Kibantu zina tabia ya kufanana kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, tofauti zinajitokeza katika majina yanayoingia katika baadhi ya ngeli za majina kati ya lugha na lugha. Hili linajitokeza pia kati ya lugha ya Kimalila na Kiswahili, jambo linalofanya nomino zinazokopwa kutoka lugha ya Kiswahili kulazimika kuingizwa katika makundi tofauti katika lugha ya Kimalila.

**Jedwali la 3.15: Mpishano wa Ngeli za Majina**

| Na. | Kiswahili | Ngeli | Neno la Mkopo | Ngeli |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Mikutano | 4 | *ámakʉtano* | 6 |
| **2.** | Sanduku | 5 | *ɨ̂nsanduka* | 9 |
| **3.** | Saba | 9/10 | *ʉʉsába* | ½ |
| **4.** | Sanduku | 5/6 | *ɨnsándʉka* | 9/10 |

Mifano hiyo inadokeza kuwa kuna baadhi ya nomino za Kiswahili zinapoingizwa katika Kimalila zinalazimika kuingia kwenye makundi tofauti ya ngeli ili kuendana na upangaji maneno katika ngeli za majina ya Kimalila. Huu ni ushahidi kuwa lugha za Kibantu hazina namna moja tu ya kuyaweka baadhi ya majina katika ngeli za majina.

#### 3.1.7.2.1Uambishaji ngeli za majina

Ngeli ya kwanza katika lugha za Kibantu ni*mu*- (Schadeberg, 2003) inayodhihirika kama *M*- au *Mw*- katika mazingira mengine kwa baadhi ya lugha kama Kiswahili (Kihore na wenzake, 2001). Wingi wa ngeli ya kwanzaunawakilishwa kwa umbo ngeli *bha*- katika lugha nyingi za Kibantu (Schadeberg, 2003), ambalo hubadilika kwa baadhi ya lugha. Hata hivyo,

lugha ya Kimalila ina tabia ya kuambisha umbo la wingi *bha* katika baadhi ya nomino zenye umbo la umoja *mu*- na kufanya maumbo yote mawili kutumika pamoja (Sote, 2020). Uambishaji huu hutokea pia wakati wa urasimishaji wa nomino zinazokopwa kutoka Kiswahili ambapo baadhi yake zinaambishwa maumbo ya ngeli mawili katika nomino moja. Hii ina maana kwamba umbo la ngeli ya umoja linachukuliwa kama sehemu ya shina la neno wakati wa ukopaji.

**Jedwali la 3.16: Uambishaji Ngeli za Majina**

| **Na.** | **Kiswahili** | | **>** | **Neno la Mkopo** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | Mw- | Alimu | > | *á* | *-bha-* | *mw-* | *Alimu* |
| | NG 1 | Alimu | | *Kat* | *NG 2* | *NG 1* | *Alimu* |
| | Mwalimu | | | *Waalimu* | | | |
| **2.** | Vi- | Jana | > | *á* | *-bha-* | *vi-* | *Jana* |
| | Ng 2 | Jana | | *Kat* | *NG 2* | *NG 2* | *Jana* |
| | Vijana | | > | *Vijana* | | | |
| **3.** | Vi- | Lanja | > | *á* | *-bha-* | *vi-* | *Lanja* |
| | NG 2 | Lanja | | *Kat* | *NG 2* | *NG 2* | *Lanja* |
| | Vilanja | | | *Vilanja* | | | |

Mifano hiyo ina maana kwamba umbo la ngeli ya 1 ya Kiswahili ni *wa*- wakati katika Kimalila ni *bha*-.Muundo wa nomino ya mkopo katika Kimalila una maumbo mawili ya ngeli: kuna umbo la ngeli 1 linalotokea jirani zaidi na shina pamoja na la ngeli ya 2 linalotokea baada ya umbo la ngeli ya 1. Katika Jedwali 3.16(2-3), maumbo mawili ya ngeli ya 2 yametokea pamoja pia. Hii inaweza kusababishwa na lugha ya Kimalila kurasimisha nomino zilizo na umbo ngeli kama sehemu ya shina. Hata hivyo, wazungumzaji wanakubaliana na

muundo wa *ábhajana,* lakini hawakubaliani kabisa na neno *ábhalanja*yaani "vilanja." Inawezekana kuwa muundo huu unatokana na tabia ya lugha ya Kimalila kuruhusu maumbo ngeli ya 1 na ya 2 kutokea pamoja kwa baadhi ya majina (Sote, 2020), ingawa maumbo ya ngeli ya 2 hayatokei pamoja katika nomino zenye asili ya Kimalila.Aidha, kuna nomino zinazokinzana na mifano katika Jedwali la 3.16 (1) kwa kuwa muundo unakuwa wa *kat* + *NG* + *shina*.

**Jedwali la 3.17: Uambishaji Ngeli za Majina**

| **1** | **Mw-** | **Anajeshi** | **>** | ***ʉ́*** | ***Mw*** | ***anajeshi*** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | NG 1 | Anajeshi | | *Kat* | *NG 1* | *anajeshi* |
| | Mwanajeshi | | | | Mwanajeshi | |
| | Wa- | Anajeshi | | *á* | *Bh* | *anajeshi* |
| | NG 2 | Anajeshi | | *Kat* | *NG 2* | *anajeshi* |
| | Wanajeshi | | | | *Wanajeshi* | |

Katika mifano hiyo, maumbo ya ngeli ya 1 na ya 2 yametokea katika Kimalila kama ilivyo katika Kiswahili. Hii ina maana kwamba lugha ya Kimalila ina namna tofauti zinazotumika kurasimisha nomino zinazokopwa katika lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo: (i) kuna muundo unaobaki kama ulivyo katika Kiswahili; (ii) kuna muundo wa ngeli ya 1 katika Kiswahili kutokea pamoja na ngeli ya 2 katika Kimalila; na (iii) kuna muundo wa ngeli ya 2 katika Kiswahili kutokea pamoja na umbo la ngeli ya 2 kwenye maneno ya mkopo katika Kimalila.

**3.1.7.2.2Uhuishaji wa ngeli ya 4**

Umbo la asili la ngeli ya 4 katika lugha za Kibantu ni*mi-* (Schadeberg, 2003), ambalo linatumika katika lugha ya

Kiswahili pia (Kihole na wenzie, 2001). Hata hivyo, lugha ya Kimalila inatumia umbo *ma*- ambalo ni la ngeli ya 6 katika nomino zenye asili ya Kimalila ambapo umbo *mi*- hutumika katika nomino za ukubwaishi. Inaonesha kwamba baadhi ya nomino za mkopo zilizo katika ngeli ya 4 zinapokelewa pamoja na umbo la ngeli ya 4 *mi*- katika lugha ya Kimalila ambalo, katika muktadha huu, linaonekana kuwa geni.

**Jedwali la 3.18: Uhuishaji wa Ngeli ya 4**

| Na. | Kiswahili | Ng | Neno la Mkopo 1 | Ng | Neno la Mkopo 2 | Ng |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | Mishikaki | **4** | *á-mashikaki* | **4** | *ɨ̂-mɨshikaki* | **4** |
| **2.** | Mitihani | 4 | *á-matinhani* | 4 | *ɨ̂-mɨtinhani* | 4 |
| **3.** | Mikate | 4 | *á-makati* | 4 | *ɨ̂-mɨkati* | 4 |
| **4.** | Mifuko | 4 | *á-mafuku* | 4 | *ɨ̂-mɨfuku* | 4 |
| **5.** | Milango | 4 | *á-malyango* | 4 | *ɨ̂-mɨlyango* | 4 |
| **6.** | Mchezo | 3 | *ʉ́-mʉchezo* | 3 | *ɨ̂mɨchezo* | |

**Ufunguo: Ng = Ngeli**

Jedwali la 3.18linaonesha kwamba ngeli ya 4 inatumia maumbo ngeli mawili ya *ma*- na *mi*- ambapo umbo ngeli *ma*- ni mahususi kwa nomino zisizo za mkopo, ilhali *mi*- linatumika katika nomino za mkopo pamoja na zisizo za mkopo. Umbo la ngeli *mi*- linatumika kwenye nomino za asili ya Kimalila katika ukubwaishi tu. Hivyo basi, inawezekana kujenga hoja kwamba maumbo ngeli ya 3/4 katika Kimalila ni*mu*- na *ma*. Umbo *mi*- linatumika katika majina yenye asili ya Kimalila lakini yaliyokubwaishwa tu; maneno ya mkopo yanatumia umbo *mi*-

tu. Hii inaweza kuwa ni ishara ya umbo *mi*- kuwa katika kipindi cha mpito cha kukubalika tena katika lugha ya Kimalila.

## 4.0 Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yameonesha namna maneno ya mkopo kutoka katika lugha ya Kiswahili yanavyorasimishwa katika lugha ya Kimalila. Zaidi pia, nomino za mkopo kutoka Kiswahili sharti zipitie mabadiliko kifonolojia au kimofolojia, ambapo matumizi ya toni pamoja na kiambishi awali tangulizi mtawalia hayaepukiki. Vilevile, sauti za irabu au konsonanti zinazoandamiana katika neno la mkopo zinachakatwa kwa kuchopeka konsonanti au irabu mtawalia. Katika mazingira mengine, miundo hii huchakatwa kwa uyeyushaji au udondoshaji wa sauti. Aidha, kuna michakato zaidi ya mitatu ianweza kufanyika wakati wa kuchakata maneno ya Kiswahili. Hii ina maana kwamba maneno ya Kiswahili hayakubaliki kirahisi katika lugha ya Kimalila. Vilevile, makala yanaonesha kwamba maneno ya mkopo yenye silabi mbili ni lazima yapitie mchakato wa urefushaji irabu katika Kimalila kwa lengo la kupata uwiano sahihi wa kizio cha chini cha mora nne katika neno. Kimofolojia, uambishaji wa kiambishi awali tangulizi katika nomino za mkopo hauepukiki katika Kimalila. Katika mazingira mengine, nomino za Kiswahili zinarasmishwa pamoja na umbo lake la ngeli jambo linalofanya maumbo mawili ya ngeli kutokea pamoja. Kwa mantiki hii, ni vigumu kurasimisha nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili katika Kimalila bila kuzifanyia maboresho yoyote kifonolojia au kimofolojia.

## Marejeleo

Bahumaid, S. (2015). Lexical borrowing: The case of English loanwords in Hadhrami Arabic. *International Journal of Language and Linguistics, 2*(6), 13–24.

Clowley, T. (1998). *Introduction to historical linguistics* (3rd ed.). Oxford: Oxford University Press.

Guthrie, M. (1967-1971). A comparative bantu: An introduction to comparative linguistics. *Prehistory of the Bantu Languages,* 4, Farnborough: Greggy Press.

Haspelmath, M. (2009). Lexical borrowing concepts and issues. www.researchgate.net/publication/279973916_Lexical_borrowing_concepts_and_issues/link/5655dd7308ae1ef9297950d9/download. Accessed on May 21, 2020.

Hock, H. H., & Joseph, B. D. (2009). *Language history, language change, and language relationship: An introduction to historical and comparative linguistics*. Berlin: Walter de Gruyter.

Hyman, L. M. (2003). Suffix ordering in Bantu: A morphocentric approach, Katika G. Booij & J. van Marle (Wah.), *Yearbook of Morphology* (p.245–281). Dordrecht: Kluwer Academic Publishers.

Kahigi, K.K. (2005). *The Sisumbwa noun: Its classes and derivation,* In Ocassional Paper in Linguistics, Series No. 1(p.117–154).

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjira, Y. P. (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI.

Kutsch-Lojenga, C. (2007). Minimality and morae in Malila (M.24), In *Selected Proceedings of 37th Annual Conference on African Linguistics*, Edited by Payne, D. L & J. Pena (p.77–87).

Lodhi, A. (2000). *Oriental influences in Swahili: A study in language and culture contacts*. Goteborg: Acta Universitatis Gothoburgensis.

Lusekelo, A. (2019). Asaption of Sukuma loanwords in the Western dialects of Datooga (Taturu) and its dialectological implications. *Ethnologia Actualis*, *19*(1), 54–89.

Lusekelo, A. (2018). Lexical borrowing in Africa with special attention to outcomes of languages in contacts in Tanzania. *Journal of African Studies*, *7*(2), 1–22.

Maganga, C., & Schadeberg, T. C. (1992). *Kinyamwezi, texts and vocabulary*. Corogne: Rudiger Koppe Verlag.

McMahon A. M. S. (1994).*Understanding language change*. Cambridge University Press.

Morrison, E. M. (2011). *A reference grammar of Bena*. Tasnifu ya Uzamivu. University of Rice.

Msuya, J., & Mreta, A.Y. (2019). Adaptation of loanwords in Chasu. *Journal of Linguistics and Language in Education*,*13*(1), 26–46.

Myers-Scotton, C. (2002).*Contact linguistica: Bilingual encounters and grammatical outcome*. Oxford: Oxford University Press.

Ngunga, A. (2002). Lexical borrowing in Ciyao. *The Journal of the Linguistics Association for Southern Africa Development Community Universities*, *1*, 15–42.

Rugemalira, J. (2005).*Runyambo Grammar*. Dar es Salaam: LOT Publications.

Schadeberg, T. C. (2003). Derivation, Katika: D. Nurse & G. Philippson (Wah.). *The Bantu Languages*. London: Routledge.

Sote, A. (2020). Uchambuzi wa maumbo ya jinsia katika nomino za kibantu: Mifano kutoka Lugha ya Kimalila nchini Tanzania. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences (RUJASS)*, *6*(1), 205–222.

Zivenge, W. (2009). *Phonological and morphological nativization of English loans in Tonga*. PhD dissertation. University of South Africa.